



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU



Unapojibu tafadhali taja:

Namba ya Zabuni: LGA/001/2023/2024/NC/01/L/1-8
Kwa ajili ya: UWAKALA WA VYANZO VYA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA
2023/2024

MWALIKO/ TANGAZO LA ZABUNI

Tarehe: 3/05/2023

1. Halmashauri ya Wilaya ya Meru inapenda kualika zabuni kutoka kwa watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa uwakala wa ukusanyaji wa mapato kutuma maombi yao kwa Zabuni hii.
2. Unaalikwa kuwasilisha Zabuni yako kwa ajili ya kukusanya Mapato ya usafi na Mazingira, mazao, maegesho na madini ya ujenzi kama ilivyoainishwa kwenye Nyaraka za Zabuni.
3. Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe Halmashauri ya Wilaya ya Meru kupitia TANEPS kabla ya tarehe 19/05/2023 saa tano kamili asubuhi. Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika kupitia TANEPS mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilishwa Zabuni.
4. Waombaji wawe na vithibitisho vya kuwa na vifaa vya kazi kama magari/ Trekta kwa ajili ya kusafirishia taka kwenda dampo, Vifaa vya kutosha vya kusafishia, wafanyakazi/vibarua wa kutosha kutokana na ukubwa wa eneo analoomba, pamoja na ofisi ya kudumu.
5. Baada ya kupata zabuni kampuni au Kikundi kiwe na Mabango makubwa ya rangi ya Kung'aa yatakayobandikwa katika magari ya kazi kwenye tela upande wa kushoto na kulia na milango ya mbele yakiwa na ujumbe wa kuhamasisha usafi, namba za simu za viongozi wa zabuni, sare za kazi za kutosha kwa wafanyakazi wote, Gum boot, Gloves ngumu za kutosha na reflector kwa wale

wote, Gum boot, Gloves ngumu za kutosha na reflector kwa wale watakaofanya usafi barabarani na ratiba za kazi kwa kila mtaa/kitongoji zipatikane kwa viongozi wa Kila mtaa/kitongoji mapato kwa wakati.

6. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Aidha, mwombaji aliyewahi kushitakiana na Halmashauri ya Wilaya ya Meru kuhusiana na kazi yeyote, hatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yeyote ya zabuni iliyotangazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Vile vile Waombaji watakaohibitika kuwa na tuhuma za utendaji usiozingatia Sheria kutoka Taasisi nyingine za Serikali hawatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi zinazotangazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru.
7. Vikundi vilivyosajiliwa kama makundi maalum (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) watapewa nafasi ya upendeleo kwenye mchakato huu kwa kupewa kazi.
8. Mwombaji lazima aweke picha yake kwenye barua ya maombi aidha Mtendaji wa kijiji/mtaa lazima athibitische uwepo wa ofisi yako sehemu ya kaz unapofanyia ili iwe rahisi wakati utakapohitajika.
9. Mzabuni atakayeshinda atalazimika kutoa risiti ya mapokezi ya EFD wakati anarejeshewa fedha yake ya 80% kulingana na mkataba hivyo kila muombaji lazima athibitische umiliki wa EFD mashine.
10. Mwombaji anatakiwa kujaza fomu kwa usahihi bila kufuta kwa kalamu au kurudishia maandishi juu ya mengine zichapwe vizuri na usighushi nyaraka yoyote ikiwepo TIN namba, Leseni ya Biashara n.k
11. Mzabuni atakayeshinda atapewa POS kwa ajili ya kukusanya mapato ambapo utatakiwa kuwa na fedha taslimuza kuwa unweka kwenye hiyo POS ili uweze kuitumia na maelekezo zaidi utapewa wakati unasaini mkataba wa utekelezaji.
12. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa kwa njia nyingine tofauti na TANEPS au zilizowasilishwa katika muundo usiokubalika na TANEPS, hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini, bila kujali mazingira yoyote.


Mkururugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Meru

